Ndugu waheshimiwa, wajuzi weledi, wanafunzi na marafiki zetu,

Baada ya salamu nyingi ni furaha yetu kubwa kutangaza kikao kifuatacho cha

**Baraza letu la Kiswahili la Berlin (BALAKI-BE) la tarehe 03 Februari 2025**

**"Kurejesha Utambulisho": Umuhimu wa Urejeshaji wa Vifaa na Elimu ya Urithi wa Kiutamaduni kwa Jamii za Tanzania**

**Flower Manase Msuya**

Katika wasilisho hili, Bi. Manase atajadili mabadiliko makubwa yaliyotokea katika jamii za Tanzania wakati wa ukoloni ambapo Tanganyika (Tanzania Bara), Rwanda, na Burundi zilikuwa koloni la Wajerumani. Utawala wa Kijerumani ulikuwa wa mabavu ukasababisha machafuko mengi na vita vya kuupinga utawala huo. Katika hali hiyo Waafrika wengi walipoteza uhai, mali, elimu, na vifaa vya urithi wa kiutamaduni. Wasilisho hili litaangazia dhana ya "urejeshaji wa utambulisho" kwa kuchambua umuhimu wa kurejesha vifaa, maarifa, na urithi wa kiutamaduni vilivyochukuliwa wakati wa ukoloni na sasa vipo Ujerumani. Mfano utakaotolewa ni wa kifaa cha kiutamaduni kiitwacho *Mwanahiti* kilichotumika kuwafundisha wasichana wa jamii za pwani kama vile Wazaramo na Wakwere.

**Bi. Flower Manase Msuya** ni mtafiti katika Makumbusho ya Taifa ya Tanzania. Ana uzoefu mkubwa katika utekelezaji wa miradi ya kitaifa na kimataifa inayohusu uhifadhi wa malikale, uandaaji wa maonesho, na utafiti wa kihistoria. Yeye ni mmojawapo wa watafiti waliopanga na kuandaa onesho la ushirikiano wa Makumbusho ya Ethnolojia Berlin, Shirika la Jukwaa la Humboldt na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania.

Kikao kitafanyika **siku ya Jumatatu, tarehe 03 Februari 2025, saa kumi na robo za Ulaya ya Kati (**saa kumi na mbili na robo za Afrika Mashariki**) kupitia njia ya Zoom:** https://us02web.zoom.us/j/87802619722?pwd=DCVrQHdFUZSAB0gjg8RuMezGyJg3Hu.1

**KARIBUNI NYOTE!**

Tafadhalini wajulisheni wapenzi wote wa Kiswahili na marafiki wengine!

Wasalaam,
Kai Kresse, Lutz Diegner na Maxwell Omondi Ondieki

*Kama kuna maswali yoyote kuhusu baraza hili tafadhalini mwandikieni mwenzetu: <MaxwellOmondi.Ondieki@zmo.de >*